UWEKAJI WA JIWE LA MSINGI KATIKA
JENGO LA MAKAO MAKUU YA MAHAKAMA JIJINI DODOMA
TAREHE 26/01/2022

Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania,

Mhe. Gerson Mdemu, Jaji Mfawidhi Dodoma,

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu,

Mhe. Naibu wa Waziri Katiba na Sheria, Geofrey M. Pinda (Mb),

Mhe. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa Dodoma,

Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,

Mhe. Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Wilbert Chuma,

Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary G. Makondo,

Viongozi wengine Waandamizi wa Serikali na Tasisi Mliopo,

Wasajili, Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama,

Mahakimu na Mawakili,

Waandishi wa Habari,

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Habari za Asubuhi,

Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetuwezesha kukutana siku hii muhimu katika historia ya Mahakama.

Leo kwangu mimi ni siku ya shukrani kwa mambo haya makubwa yanayoendelea kufanyika katika jiji hili la Dodoma, nianze kwa kuishuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama, hadi kufikia hatua hii mnayoiona hii leo.

Shukran kwa Wasimamizi wa Ujenzi

Naomba kuwashuru wasimamizi wa ujenzi kutoka ndani ya Mahakama, Mtaalam Mshauri na Mkandarasi kwa kazi nzuri inayoendelea kutekeleza.

Naishukuru sana Serikali kwa kutoa kibali kwa Mahakama ya Tanzania kutohamia Dodoma hadi jengo hili litakapokuwa limekamilika.

Mhimili wa Mahakama Bila Jengo lake la Makao Makuu

Mwezi Aprili mwaka 2017, mwandishi wa gazeti la DAILY NEWS, Bw. Nicodemus Ikonko alifanya mahojiano na Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman. Katika toleo la tarehe 02 Aprili, 2017 linaonyesha kuwa moja ya maswali aliyomuuliza Mheshimiwa Mohamed Chande Othman, ni jambo gani ambalo alipenda kulikamilisha lakini hakuweza, na angependa likamilike.

Alijibu kuwa alisikitika kuiacha Mhimili wa Mahakama ambao hauna jengo rasmi la Makao Makuu. Aliendelea kuonyesha kusononeshwa na hali ya Mahakama ya Rufani bado kuendelea kutumia jengo ambalo ni KLABU ya zamani ya wakoloni (Dar es Salaam Club), ambalo usanifu wake haukuwa na malengo ya matumizi ya Mahakama. Hapa aliiomba Serikali itimize ahadi yake na iiwezeshe Mhimili wa Mahakama ili nao upate Makao Makuu yake.

Kabla ya uamuzi wa Serikali kuhamisha Makao Makuu ya Nchi kutoka Dar es Salaam hadi Dodoima, Mahakama ya Tanzania ilipanga kujenga Makao yake Makuu katika Kiwanja kidogo pale Mtaa wa Chimala. Michoro ilikuwa tayari na kilichobaki ilikuwa

kutafuta kandarasi wa kuanza ujenzi. Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania haukuendelea katika kiwanja cha Chimala jijini Dar es Salaam.

Kiwanja cha Makao Makuu ya Mahakama Dodoma

Historia ya kupata kiwanja cha ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania, Dodoma, eneo la NCC ilianza mwezi Disemba 2017. Nakumbuka ilikuwa tarehe 07/12/2017 aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alinialika huko Ikulu ya Chamwino Dodoma.

Baada ya mazungumzo, Mhe. Rais akaagiza Uongozi wa iliyokuwa Manispaa ya Dodoma (kabla ya kutangazwa kuwa Jiji) utafute kiwanja ili Mahakama ya Tanzania ijenge Makao Makuu ya Mahakama jijini Dodoma.

Uongozi wa Manispaa ya Dodoma chini ya Mkurugenzi Ndg. Godwin Kunambi (sasa ni Mbunge wa Mlimba) ulitafuta maeneo mawili kwa ajili ya Mahakama kuchagua moja wapo kwa ajili ya Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania.

Jaji Mkuu na Jaji Kiongozi wa wakati huo, Mhe. Jaji Ferdinand Wambali (sasa JR), Jaji Mfawidhi Dodoma wa wakati huo, Mhe. Jaji Mwanaisha Kwariko (sasa JR)—walitembelea maeneo hayo mawili wakiwa pamoja na Bw. Kunambi:

(a) Eneo la Chimwaga lenye Hekta 50; na

(b) Eneo la NCC lenye ukubwa wa 18.9 hekta.

Baada ya maeneo hayo mawili kufanyiwa tathmini za kijiolojia, Mahakama ilichagua eneo la NCC lenye Hekta **18.9**. Eneo hili lipo hapa NCC LINK katika Kiwanja Namba 1 KITALU "D". Kuna mambo kadhaa yalifanyika kabla ya ujenzi kuanza:

(i) Kupima na kupata rasmi miliki Namba 36606 DRL.

(ii) Kuweka mipaka inayoonekana ili kuondoa uwezekano wa kuingiliwa au eneo kuvamiwa.

(iii) Kuchonga USHOROBA (CORRIDOR) kuzunguka eneo lote.

(iv) Kupanda miti ya vivuli kuzunguka eneo lote.

(v) Eneo hili lilifanyiwa vipimo vya kisayansi kwa kutumia wataalamu kutoka WAKALA WA JEOLOJIA.

(vi) Eneo limefanyiwa pia "Topographic-survey."

Haya yote yamesaidia wataalamu wa michoro kuzingatia hali halisi kwenye michoro.

Kwa nini Mahakama iliteua eneo la NCC Dodoma

Pamoja na kuwa eneo dogo kuliko la Chimwaga, uongozi wa Mahakama uliona eneo lenye Hekta **18.9** linakidhi mahitaji ya Mahakama kujenga Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania, Makao Makuu ya Mahakama ya Juu *(Supreme Court)* endapo itaanzishwa, Makao Makuu ya Mahakama ya Rufani, Makao Makuu ya Mahakama Kuu na Makao Makuu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Eneo linatimiza sharti muhimu alilolitoa Mhe. Rais, la kuwa na heshima, taswira na hadhi ya Mahakama kama mmoja wa Mihimili mitatu ya Dola.

Muonekano wake ni mzuri kutoka mbali na kielelezo kizuri kwa wananchi kuwa Mhimili wa Mahakama kuonekana kutoka mbali. Kiwanja kina sifa ya ukaribu na kiwanja ambacho jengo jipya la Mahakama Kuu (Jumuishi au *IJC*) Dodoma lililozinduliwa na Mhe Rais Samia Suluhu Hassan tarehe 6 Oktoba 2021.

Kiwanja kipo karibu na Taasisi nyingi kama vile Benki Kuu, Wizara ya Fedha. Kwa kuwa Mahakama hutoa huduma kwa wananchi, ukaribu na jiji la Dodoma hususan sehemu wanazoishi wananchi wengi ilizingatiwa.

Eneo linafikika kwa urahisi kwa vile limezungukwa na barabara katika pande zote nne, hivyo ni rahisi kuingilika kila upande. Njia ya Reli ya SGR inapitia karibu na jengo. Miundo mbinu ya maji safi na maji taka, pamoja na umeme ipo karibu.

Baada ya tathmini ya wataalamu wa Jiolojia, ilionekana kuwa vitovu vya matetemeko ya ardhi (*earth quake epi-centres*) yaliyowahi kutokea Dodoma yapo mbali na kiwanja takriban kilometa kumi (10) kutoka eneo la jengo.

Eneo kiwanja cha Makao Makuu ni kubwa kiasi cha kutoa nafasi kwa matumizi ya baadaye. Aidha, eneo hili sio kubwa sana kiasi cha kuonekaa kuhodhi maeneo makubwa yasiyotumika kwa muda mrefu.

Jengo hili ni la gharama kubwa

Napenda kutambua kuwa hili jengo, lililoanza kujengwa tarehe 08 Julai, 2020, linasimama ndani ya eneo la MITA MRABA **55,220**. ni la gharama kubwa katika historia ya Mahakama ya Tanzania. Gharama ya Shilingi **BILIONI 129.7** (**TZS. 129,740,285/=**) sio kiasi kidogo kutengwa na Serikali kujenga Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania. Hili jengo ni utekelezaji wa AHADI ya Serikali kuiwezesha Mahakama ya Tanzania, kuwa na Makao Makuu yenye hadhi na ubora wa kimataifa.

Na hata waliohusika kufanikisha ujenzi, wana sifa na ushindani wa kimataifa. Kwa mfano, Wakala wa Jeolojia, Wataalamu wa Michoro, Kampuni ya ushauri (ARQUES AFRICA); na Mkandarasi [CRJE (East Africa)]—wote hawa wana sifa za ushindani wa kimaifa, na nina Imani kuwa hili jengo litakuwa katika WASIFU WAO (CV) kwa muda mrefu sana ujao.

Aidha Serikali imeendelea kutoa fedha za utekelezaji wa mradi huu kwa ufanisi mkubwa. Mpaka sasa Mkandarasi ana HATI ZA

MALIPO YA HAZINA (CERTIFICATE) mbili (2) tu zilizoko kwenye mchakato wa malipo.

Kutokana na heshima na hadhi ya jengo hili, natoa rai kwa wasimamizi wote wa mradi huu kuwa makini zaidi katika hatua za ukamilishaji wa jengo hili ili azma na kiu ya miaka mingi ya Mahakama ya Tanzania iwe na Makao Makuu itimizwe kwa ufanisi wa hali ya juu.

Hatua ya umaliziaji ina changamoto nyingi kwa hiyo wadau wote wa utekelezaji wa mradi huu wajipange kukabiliana nazo ili tupate jengo zuri litakaloongezea jiji la Dodoma mng'aro wa Makao Makuu ya nchi.

Matayarisho ya Samani

Jengo limefikia hatua ambayo tunahitaji kuanza matayarisho ya samani ili jengo likikamilika, lianze kutumika mara moja. Nimuomba Mtendaji Mkuu wa Mahakama aanze maandalizi ya mapema ya samani za jengo hili ili likikamilika tu lianze kutumika.

Maandali hayo ya samani yanapaswa mapema ili kuwapa wazabuni wataoshinda zabuni muda wa kutosha ili waweze kupata samani zenye kiwango cha ubora wa hali ya juu, unaofanana na hadhi ya jengo.

Utayari wa samani uende sambamba na utayari wa jengo hili kuwa kitovu cha Mahakama Mtandao. Jengo hili liwe na utayari kutumia teknolojia za mapinduzi ya nne ya viwanda.

Kutayarisha Watumishi wa Jengo hili

Matayarisho yafanyike kuwapata watumishi wenye fikra na mitizamo ya utoaji huduma kulingana sio tu na hadhi ya jengo, bali wawe na uwezo wa kutoa huduma katika Mahakama Mtandao.

Matayarisho ya watumishi watakaotoa huduma katika jengo hili la kisasa na wanaopaswa kuhamia Dodoma, waanze kuandaliwa sasa kisaikolojia ili Desema 2022 ikifika isionekana kama jambo ambalo walikuwa hawalijui.

Mwisho niendelee kuwaomba viongozi wa Mahakama wanaohusika katika jengo hili. Ubora na hadhi ya jengo inategemea pia mandhari mazuri, yenye miti ya kutosha, majani mazuri na mitaro inayopeleka maji ya mvua sehemu zinazostahili.

Viwanja vya michezo vitakavyojengwa viwe na hadhi inayolingana na jengo hili. Tupate jengo bora lenye mandhari ya kuvutia. Hatua tuliyofikia tunahitaji kuimarisha usimamizi, mashauriano na ushirikiano wa hali ya juu.

Asanteni kwa kunisikiliza na nawatakia kazi njema.